# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA WILAYA MBOZI-SONGWE

## SHULE YA SEKONDARI SIMBEGA

**Mawasiliano**

**Mkuu wa shule : 0762-414611**
**Makamu mkuu wa shule :0625-711260**

**Patron: 0764-712706**

**SHULE YA SEKONDARI SIMBEGA**

**S.L.P 99**

**MBOZI-SONGWE**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SIMBEGA-2023

**14.06.2023.**



\

**MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**
**……………………………………………….........**
**S.L.P ………………………………………........**
**……………………………………………........**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI SIMBEGA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOZI MKOA WA SONGWE MWAKA 2023.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2023** na atasoma tahasusi ya ………….

Shule hii ipo katika Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe. Ipo kilomita 14 kutoka kituo kiitwacho Njiapanda ya Iyula, Barabara kuu ya Mbeya- Tunduma. Kama unatokea njia ya Dar es Salaam, Dodoma au Iringa na umepanda gari inayoishia Mbeya, teremka Stendi ya Nanenane au Stendi kuu ya Mabasi jijini Mbeya kisha panda daladala kuelekea stendi kuu ya mabasi madogo iliyoko uwanja wa ndege wa zamani maarufu kama Airport ya zamani kwa gharama ya T.Shs 500/= tu, kisha panda gari za Tunduma (Coaster) kwa nauli ya T.Shs. 3,000/= tu kisha shuka kituo kiitwacho Njiapanda ya Iyula na panda usafiri aina ya Noah kwa shilingi 3,000/= au Pikipiki kwa shilingi 5,000/= na ushukie kijiji cha Iyula "A" . Ukitokea njia ya Sumbawanga shuka njiapanda ya Iyula kisha panda usafiri aina ya Noah kwa shilingi 3,000/= au Pikipiki kwa shilingi 5,000/=.
Aidha, kama unatokea Dodoma au Dar es Salaam kuna mabasi ya Tunduma moja kwa moja. Ukitumia hayo, omba kushushwa katika kituo cha Njiapanda ya Iyula.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **14.08.2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13.08.2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31.08.2023**

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -**

**2.1 SARE ZA SHULE:**

Sare ya shule hii ni kama zifuatazo:
i. Suruali mbili,1 Dark bluu,1 nyeusi, upana miguuni inchi 18 yenye pindo chini. (turn up).
ii. Mashati meupe mawili yenye mikono mirefu.
iii. Jezi (bukta na fulana) rangi ya bluu bahari pamoja na viatu vya michezo.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya ngozi na vya kufunga na kamba, vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali usio na chuma kubwa wala picha



\

vii. Sweta rangi ya kijani(Pia linapatikana kwenye duka la shule kwa Tsh 15,000/=)
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni suruali mbili rangi ya damu ya mzee na ix.T-shirt moja ya kijani..
ix. T. Shirt 1 ya kola rangi ya kijivu kwa ajili ya kuvaa darasani (Pia inapatikana kwenye duka la shule kwa Tshs. 15,000 tu).
x. Track suit – nyeusi isiyo na maandishi.
xi. Kandambili kwa ajili ya kuogea

**2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:-**

i. Madaftari 08 (counter Book-Quire 4)
ii. Ream Mbili (2) (A4) kwa mwaka.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatanishwa*);
iv. Scientific Calculator 1
v. Godoro imara la futi mbili na nusu kwa sita.
v. Shuka 2 rangi ya bluu, blanket 1, chandarua 1 rangi ya bluu.
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.
x. Tochi moja kwa ajili ya dharula umeme unapokosekana.

**2.3 MICHANGO MBALIMBALI**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha za michango tajwa hapo juu zilipwe kwenye akaunti ya shule: **SCHOOL RECURRENT ACCOUNT,SIMBEGA SEC:Ac.no. 6120110009 NMB**(Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo



\

yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**NB.Kwa kuwa mwanafunzi haruhusiwi kumiliki line/simu,shule imeweka utaratibu kwa wazazi/walezi kuwatumia watoto wao fedha ya matumizi kupitia simu 0756342983/0764712706/0753123274**



\

### 3.2. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu na nywele;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha tatu (3) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v.orodha ya vitabu muhimu vinavyotumika shuleni.

***Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SIMBEGA**

**………………………**

**FRANGSON KAJANGE MKATEGE**
**MKUU WA SHULE**



\

NB:  Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. Tafadhali upatapo ujumbe wowote kuhusu mwanafunzi/mtoto wako usitume chochote, ni vema ukawasiliana na uongozi wa shule kupata ukweli wa taarifa husika kwa namba zifuatazo**: -**

- MKUU WA SHULE: 0762-414611/ 0622-704766
- MAKAMU MKUU WA SHULE: 0753-123274/0625-711260
- MWANDAMIZI TAALUMA: 0629-662818.
- MWANDAMIZI MALEZI: 0756-342983**.**



\

**APPENDIX: A**

PRESIDENT'S OFFICE,
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
SIMBEGA SECONDARY SCHOOL

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

FROM THE HEADMASTER,
SIMBEGA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 99,
**MBOZI-SONGWE.**

To THE MEDICAL OFFICER
Name of Student…………………………………………………..(Full name)
Please examine the above named student as to his physical and mental fitness for a full time student.
The examination should include the following categories (1-3)

1. a. Hearing b. Speech c. Limbs d. Eyesight e. Leprosy f. Epilepsy and g. General diseases.
2. Neurosis.
3. Other Serious diseases e.g. TB etc

**MEDICAL CERTIFICATION**

a. Hearing…………………………………………………………………..
b. Speech…………………………………………………………………..
c. Limbs……………………………………………………………………
d. Eyesight…………………………………………………………………..
e. Leprosy ………………………………………………………………
f. Epilepsy ………………………………
g. Other diseases e.g. T.B……………………………………………………..
………………………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………….
Comment……………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………….
Name………………………………..Signature………………Date……………….
Station……………………………………………Designation………………….



\

**KIAMBATANISHO B.**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI SIMBEGA**
**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE**

1. Jina kamili la mwanafunzi……………………..……………………………………………
2. Anuani ya nyumbani S.L.P…………………Wilaya……………………………………..
3. Mahali alipozaliwa Kijiji/Mtaa………………Kata………………....Tarafa…..................
4. Mahali unapoishi kwa sasa: Kijiji/Mtaa………………Kata……….Tarafa……….......
   Wilaya……………………Mkoa………………………………..
5. Shule ya Sekondari uliyotoka/kumalizia kidato cha nne………………………………..
6. Dini/Dhehebu lako…………………………………Kabila……………………………
7. Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu kwa masuala ya shule:
   i.Jina kamili la Baba………………………………………..Simu………………………
   Hai/Si hai…………………Kama hai, kazi yake………………………………………
   ii. Jina kamili la Mama………………………………………..Simu……………………
   Hai/Si hai…………………Kama hai, kazi yake………………………………………….
   Anwani S.L.P…………………………Wilaya…………………………………………..
   **Bandika picha za watajwa hapo juu kwenye vijisanduku kama wapo hai**

| **BABA MZAZI** | **MAMA MZAZI** | **MLEZI** |
|---|---|---|

**AHADI YA MWANAFUNZI:**

Mimi Mwanafunzi………………………………………………..nakubali kwa dhati nafasi niliyopewa na Taifa langu kujiunga na Shule ya Sekondari Simbega na nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa ni za kweli. Pia, ninaahidi kufuata sheria zote za shule kama zilivyotolewa na Uongozi wa Shule.

…………………………
SAINI YA MWANAFUNZI

………………
TAREHE



\

**KIAMBATANISHO C.**

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi Mzazi ……………………………………………………………………….naahidi kwamba nitatimiza wajibu wangu kwa mwanangu na kumsisitiza kufuata taratibu zote za shule kama ilivyoelekezwa na itakavyoelekezwa na uongozi wa shule ili kumpa mwanangu malezi bora yatakayomwezesha kuwa raia mwema na bora wa Taifa letu.

……………………………………..                                        …………………………

Saini ya Mazazi/Mlezi                                        Tarehe



\

## KIAMBATANISHO D.

## VIFUATAVYO NI BAADHI YA VITABU VINAVYOTUMIKA SHULENI

Mwanafunzi anashauriwa kununua vitabu kulingana na masomo yake kwa kufuata mchanganuo ufuatao:

| | |
|---|---|
| **GENERAL STUDIES**<br>1.Understanding General Studies For Advanced level (5&6) by Joannes Bigirwamungu & Sospeter M. Deogratius<br>2. General Studies Alive (5 & 6) by Zisti Kamili (2017)<br>3. General Studies Notes: Current syllabus Approach form 5 & 6 by Nyambari Nyangwine, G.M Zombwe, Godfrey Mshiu & James Egino. | **HISTORY**<br>1.Advanced Learning Word History by Idrisa Msuya book 1 & 2<br>2.Essentials in Advanced Level History paper 1 & 2 by Saleh Yasin<br>3. Advanced Level History 1 & 2 by K. Shibitali<br>4. Medieval Ages paper 2 by M. Mavunde |
| **ECONOMICS**<br>1. Economics 1 & 2 by Tayebwa Mgisha<br>2. Modern Economics Theory by Dewelt<br>3. Essential Economics 1 & 2 by Odhiambo<br>4. Modern Economics 20th Edition by Ahuja<br>5. Comprehensive of Economics Questions and Answers by Tayebwa. | **ACCOUNTANCY**<br>1. Advanced Accounting I & II, 10th Edition by Frank Wood |

| | |
|---|---|
| **BASIC APPLIED MATHEMATICS**<br>1.Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools form V by Septine I. Sillem, 2014<br>2. Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary Schools form VI by Septine I. Sillem, 2014<br>3. Basic Applied Mathematics for Advanced Level Secondary Schools form five and six by TIE | **GEOGRAPHY**<br>1.Integrated Approach in Geography by David Waugh (2009) 3rd edition<br>2. A comprehensive Approach in Physical Geography by D.T Msabila (2018)<br>3. Practical Geography by Zisti Kamili 2nd Edition 2016<br>4. Complementary Physical Geography for Secondary school by O. Mpalaki & F.Lighuda |
| **COMMERCE**<br>1. New Trend in Commerce by AbdulLatif Katende<br>2. Textbook of Commerce by Dina Kamasanyu<br>3.Simplified Commerce by Saleemi. | |



\